# KATIBA YA KIKUNDI CHA

……………………………………………………………………

# KATA YA KIKOMBO

# MTAA WA

……………………………………………………………

**KATIBA YA KIKUNDI CHA ………………………………………………………….**

**SURA YA KWANZA**

**1.0. UTANGULIZI:**

…………………………………….Ni kikundi cha hiari chenye lengo la kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa ustawi wa wanachama wake. Kikundi hiki kimeanzishwa rasmi tarehe........................... Kikundi hiki kina jumla ya Wanachama…………………….

Pamoja na Katiba hii, Kikundi hiki kitaendeshwa kwa mujibu wa kanuni mbalimbali ambazo zitawekwa na wanachama.

**1.1. Taarifa za Kikundi**

1.2. Jina la Kikundi:……………………………………..

1.3. Eneo Kilipo: Kata……………Mtaaa………………

1.4. Anuani:………………………………………………

1.5. Simu: ……………………………………………….

**1.2. Tafsiri**

Kwa mujibu wa Katiba hii, maneno yafuatayo yatakuwa na maana ifuatayo;

i. Mwanachama: Mtu yeyote atakayekidhi vigezo vya kuwa mwanachama

ii. Mwanachama hai: Mwanachama anayetimiza masharti ya kuwa mwanachama kwa mujibu wa katiba hii.

iii. Kanuni: Muongozo wa jinsi ya uendendeshaji wa kikundi

iv. Kikundi: Taasisi hii inayoanzishwa kwa mujibu wa katiba ambayo inatambulika kuwa ni Kikundi.

v. Nidhamu: Kitendo chochote kile kinacho kinzana na Katiba hii pamoja na kanuni zake.

**SURA YA PILI**

***2.0. MADHUMUNI NA MATARAJIO YA KIKUNDI***

**2.1. Aina ya Kikundi**

………………………………. ni Kikundi cha Kijamii na Kiuchumi (Community Based Organisation)

## 2.2 Madhumuni ya Kikundi.

Kikundi hiki kipo kwa kutimiza au kutekeleza yafuatayo..

a. Kushirikiana kufanya miradi mbalimbali ya Kiuchumi na Kijamii kwa maendeleo ya kikundi na ustawi wa wanachama

b. Kuanzisha mfuko wa kikundi wa kuweka na kukopa.

c. Kushirikiana na kusaidiana nyakati za shida na raha.

d. Wanakikundi kuwezeshana katika kuimarisha hali zao za Kipato ili kuweza kuwa na maisha yaliyo bora zaidi.

e. Kuwezesha kifedha shughuli binafsi za Wanakikundi mmoja mmoja kwa kuzingatia Masharti na Kanuni zitakazokuwa zimeafikiwa na Wanakikundi wote.

## *2.3. Matarajio ya Kikundi*

Ili kuweza kufikia matarajio ya Kikundi kitafanya yafuatayo:-

i. Kuweka utaratibu mahsusi wa kukusanya MICHANGO YA FEDHA kutoka kwa wanakikundi ikiwa ndio msingi wa chanzo cha mapato.

ii. ubuni Miradi mbalimbali itakayosimamiwa na kuendeshwa Wanakikundi wenyewe au hata kwa msaada wa kiufundi kutoka nje ya kikundi.

iii. Kuweza kuandaa maandiko ya kuwezesha kuomba MISAADA kutoka kwa Washirika mbalimbali wa Maendeleo wa ndani na nje ya Tanzania.

iv. Kuimarisha Ushirikiano na Wanakikundi wenye changamoto mbalimbali kama vile; Maradhi, Misiba, Harusi na Sherehe, Majanga ya Kiasili na matukio mengine yanayolingana na hayo.

## *2.4 Mradi/Shughuli za Kikundi*

Kikundi hiki kinajishughulisha na-

i. ………………………………………………

ii. …………………………………………………. Etc

Pia Kila mwanakikundi anatekeleza Mradi wake

# *SURA YA TATU*

## *3.0 UANACHAMA.*

Kutakuwa na aina mbili zifuatazo za uanachama ambazo ni;

### *3.1.1. Mwanachama wa Kawaida*

Ni mtu yeyote yule ambaye ametimiza taratibu zote za kujiunga na Kikundi au Umoja huu kwa mujibu wa Katiba na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na kulipa Ada na Michango stahiki.

### *3.1.2. Mwanachama wa Kutunukiwa*

Mwanachama wa Kutunukiwa ni Mtu yeyote atakaetunukiwa uanachama kupitia maamuzi au azimio la Mkutano Mkuu katika kuthamini Mchango uliotolewa na Mtu huyo ama atakaoendelea kuutoa kwa kuleta maendeleo na ufanisi wa Malengo ya Kikundi au Umoja huu.

### *3.2. Sifa za kuwa Mwanachama*

i. Awe na Umri usiopungua miaka 18.

ii. Awe mwenye nia na awe tayari kuwa mwanachama

iii. Awe tayari kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kikundi

iv. Awe na akili timamu.

v. Awe tayari kutii na kufuata masharti ambayo yameainishwa kwenye Katiba na Kanuni za kikundi

vi. Awe tayari kulipa kiingilio pamoja na ada ya uanachama ya kila mwezi

### *3.3. Haki za Mwanachama*

a. Kutoa maoni yake kwa uhuru

b. Kuchagua au kuchaguliwa katika nafasi yoyote ile ya Uongozi katika Kikundi au Umoja huu.

c. Kuwasiliana na Uongozi/Viongozi ikiwa ni pamoja na kupokea na kutoa taarifa zinazohusu Kikundi au Umoja huu.

d. Kuhudhuria na/au kuwakilisha katika jambo lolote lile linalohusu Kikundi au Umoja huu kwa kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba hii.

e. Kupewa nafasi ya kujieleza na kujitetea pindi anapokabiliwa na tuhuma zozote zile dhidi yake katika umoja huu.

f. Kutumia Mali za Kikundi kwa kufuata utaratibu na Kanuni za Umoja huu.

g. Ana haki ya kutoa hoja yake na kusikilizwa wakati wa kushiriki majadiliano kwenye vikao.

h. Kufahamu mapato na matumizi ya Kikundi kwa kutumia na kuzingatia Kanuni.

i. Kusaidiwa linapomtokea tatizo.

j. Kusaidiwa kimawazo au kiuchumi kulingana na hali itakavyo ruhusu.

### *3.4. Wajibu wa Mwanachama.*

a) Kalinda na kuitetea katiba hii wakati wote.

b) Kutekeleza majukumu atakayopewa na viongozi au wanachama wenzake.

c) Kushiriki katika shughuli zote za kikundi kwa mujibu wa katiba hii ikiwa ni pamoja na vikao halali vya Kikundi.

d) Kulipa ada pamoja na michango mbalimbali itakayo pitishwa na Kikundi.

e) Kueneza sifa nzuri za Katiba.

f) Kutii na kufuata maagizo na maazimio ya Mkutano/Mikutano halali ya Kikundi hata ikiwa hatakuwepo kwenye Mkutano huo, au hakushiriki katika kupitisha azimio hilo.

g) Kuwa na nidhamu wakati wa Mikutano ama shuhuli nyingine zozote za Kikundi.

h) Kutunza siri zote za Kikundi

***3.5. Kujiunga na Kikundi.***

Baada ya wanachama kujiunga na kukubaliana watalazimika kulipa kiingilio na michango ama ada ya kila mwezi.

***3.6. Michango***

(a) Ada ya Uanachama

Kila Mwanachama atalazimika kulipa kiingilio na ada ya Uanachama kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 3.5. ya Katiba hii.

ILI MRADI IELEWEKE KWAMBA:-

Mwanachama ambaye alikuwa na taarifa juu ya uanzishwaji wa kikundi na hakujiunga wakati huo, endapo atataka kujiunga baadae, atatakiwa kulipa kiingilio na michango yote tangu kikundi kilipoanza mpaka kilipofikia, ndipo ataweza kukubaliwa kuwa mwanachama.

(b) Michango Mingineyo.

Kila Mwanachama atawajibika kuwasilisha mchango mwingine wowote ule utakaoamuliwa kuchangishwa kwa azma ya kukidhi miongoni mwa matarajio ya Kikundi kama yalivyoainishwa katika ibara 2.3 ya Katiba hii na kima kitakachokuwa kimeamuliwa.

(c) Michango ya Hiari

Kutakuwa na michango ya hiari ambayo mtu hatolazimishwa bali anaweza kujitolea mali au fedha kwa mapenzi yake mwenyewe kwa lengo la kukijenga na kukiendeleza Kikundi.

***3.7. Kukoma Uanachama.***

Mwanachama anaweza kukoma kuwa mwanachama katika mazingira yafuatayo:-

a. Kujitoa kwa hiari yake kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mwenyekiti wiki moja kabla na kama ana mali za Kikundi atalazimika kurudisha ndipo atakubaliwa kutoka, lakini hatorudishiwa michango au mali yoyote aliyoitoa kwa ajili ya Kikundi.

b. Kushindwa kulipia ada ya kila mwezi kwa miezi mitatu mfululizo bila sababu yoyote ya msingi.

c. Kutohudhuria bila taarifa vikao vitatu mfululizo vilivyowekwa kwa mujibu wa katiba hii bila sababu ya msingi.

d. Kupuuza taarifa zinazotaka ushiriki wake katika shughuli za wanachama.

e. Kupoteza sifa kutokana na mambo ya kinidhamu

f. Ikiwa mwanachama atafariki.

g. Kushidwa kufuata Katiba na Kanuni za Kikundi.

ILI MRADI IELEWEKE KUWA

Mtu aliyeacha au kufukuzwa Uanachama (uanakikundi) anaweza kuomba kujiunga tena kwa mujibu wa masharti ya uanakikundi baadae na atatakiwa kuwa na wadhamini wasiopungua WATATU ndani ya Kikundi ambao ni hai.

NA

Kama mwanachama atakoma kutokana na vigezo tajwa hapo juu, atakuwa amepoteza haki zake zote za msingi kama mwanachama.

## SURA YA NNE.

### *4.0. UONGOZI.*

### *4.1. Aina za Viongozi*

Kikundi hiki kitakuwa na viongozi wafuatao:-

(i) Mwenyekiti

(ii) Makamu Mwenyekiti

(iii) Katibu

(iv) Katibu Msaidizi

(v) Mweka Hazina

(iv) Wajumbe wawili watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu kama Kamati ya Nidhamu.

## SURA YA TANO.

### *5.0. KAZI ZA VIONGOZI*

### *5.1. Kazi za Mwenyekiti.*

1. Atakuwa msemaji mkuu wa kikundi.

2. Ataitisha mikutano yote ya kikundi.

3. Ataitisha mkutano wa dharura pale itakapokuwa inahitajika.

4. Ataongoza mikutano yote ya wanachama wote.

5. Atakuwa ndio Kiongozi Mkuu wa Kikundi au Umoja huu.

***5.2. Kazi za Makamu Mwenyekiti.***

I. Atafanya kazi zote za Mwenyekiti pale ambapo Mwenyekiti hatakuwepo.

II. Atafanyakazi zote atakazoelekezwa na Mwenyekiti.

III. Atakuwa ndio msaidizi mkuu wa Mwenyekiti.

***5.3. Kazi za Katibu.***

i) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa kikundi.

ii) Kuandaa ajenda za vikao vyote.

iii) Ataandika miniti za vikao vyote vya kikundi.

iv) Atakuwa anatoa taarifa ya maendeleo ya kikundi mara moja kwa mwezi

v) Kwa kushirikiana na Mwenyekiti atakuwa anaandaa yatokanayo na vikao vilivyopita

vi) Atakuwa mtunza kumbukumbu na nyaraka mbalimbali za kikundi.

vii) Atakuwa katibu wa kamati ya utendaji.

viii) Atakuwa mjumbe wa kamati ya Fedha na Mipango.

ix) Atawajulisha wanachama taarifa zote za vikao.

x) Atafanya kazi zote kadri atakavyoelekezwa na Mwenyekiti.

***5.4 Kazi za Katibu Msaidizi.***

i. Atamsaidia Katibu kuendesha shughuli za kila siku za kikundi.

ii. Atakaimu nafasi ya Katibu pale ambapo Katibu atakuwa hayupo.

***5.5. Kazi za Mweka Hazina.***

i. Atakuwa mtunza fedha za kikundi.

ii. Atakusanya / atapokea fedha zote za kikundi na kutoa stakabadhi.

iii. Atakuwa mtunza nyaraka zote zinazohusiana na masuala ya fedha.

iv. Atatoa taarifa ya mapato na matumizi ya kikundi kila miezi mitatu.

v. Atafanya malipo yote halali ya kikundi.

vi. Atajibu hoja zote zinazo husiana na masuala ya fedha.

vii. Atakuwa mjumbe wa kamati ya utendaji pamoja na kamati ya Fedha na Mipango.

***5.6. Kamati ya Nidhamu***

a) Kamati hii itakuwa na jukumu la kusimamia nidhamu na kushughulikia migogoro ya wanachama. Kamati hii itaundwa na wajumbe wawili watakaoteuliwa na wana kikundi. Mwenyekiti wake kama itawezekana awe ni mtu mwenye busara na ufahamu wa katiba ya kikundi. Kama hatakuwepo mtu wa kukidhi kigezo hicho, mtu mwingine yeyote atakayeteuliwa na wanakamati wenyewe ndio atakuwa Mwenyekiti.

b) Migogoro yote ya kikundi kwanza inatakiwa wasikilizwe na kamati ya nidhamu na kusikilizwa ndani ya muda wa wiki moja toka siku ya lalamiko lilipowasilishwa

c) Ikitokea mkutano mkuu wa kikundi umeshindwa kutatua mgogoro uwasilishwe kwa Afiasa Maendeleo ya jamii ngazi ya Kata

d) Afisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata akishindwa kutatua Mgogoro uwasilishwe katika Ofisi ya Mkurugenzi, Divisheni ya Maendeleo ya Jamii.

e) Ngazi zote wakishindwa kutatua mgogoro ufikishwe mahakamani

**SURA YA SITA.**

***6.0 MIKUTANO/ VIKAO***

Kikundi hiki kitaongozwa kwa kufanya vikao mbali mbali kama vifuatavyo.

***6.1 Mkutano Mkuu***

Kutakuwa na mkutano mkuu utakaofanyika mara moja kwa mwaka. Ili mkutano huu ufanyike idadi ya wajumbe watakohudhuria kikao hicho ni lazima iwe siyo chini ya asililimia TISINI (90%) ya wajumbe wote walio hai

***6.2 Kazi za Mkutano Mkuu.***

(i) Kuchagua viongozi wa kikundi.

(ii) Kupokea taarifa za mapato na matumizi kwa mwaka mzima.

(iii) Kupokea taarifa ya kazi zote za mwaka.

(iv) Kufanya mabadiliko au marekebisho kwenye vifungu mbalimbali vya katiba.

(v) Kuidhinisha mipango ya kimaendeleo ya kikundi

(vi) Kufanya Uchaguzi wa viongozi ikiwa muda umewadia.

***6.3 Mkutano wa Kawaida wa Wanachama Wote.***

1) Mkutano huu utafanyika mara moja kwa mwezi, siku na tarehe zitajulishwa na katibu wiki moja kabla.

2) Ili mkutano huu ufanyike ni lazima idadi ya wajumbe ifikie asililimia 90% ya wajumbe wote walio hai. Endapo kikao kitasitishwa mara mbili kwa kukosa akidi, kikao cha tatu kitaendelea hata kama akidi itakuwa haijafikiwa na maamuzi ya kikao yatakuwa maamuzi halali ya kikundi.

### *6.4 Kazi za Mkutano wa Kawaida wa Wanachama Wote.*

(i) Kupokea taarifa ya utendaji na uendeshaji kikundi kwa mwezi husika.

(ii) Kukusanya michango ya kila mwezi toka kwa wanachama.

(iii) Kupata taarifa za utekelezaji wa maagizo na malengo yoyote ya kikundi.

(iv) Kupokea taarifa ya fedha ya mwezi husika.

(v) Kupitisha maamuzi ya kamati mbalimbali za kikundi.

(vi) Kujadili na kulitolea uamuzi suala lolote litakalokuwa limejitokeza.

(vii) Kupanga tarehe na sura ya kufanyia mkutano wa mwezi unaofuata.

## SURA YA SABA

### *7.0 TARATIBU ZA UCHAGUZI*

Kutakuwa na chaguzi mbali mbali za viongozi wa kikundi, ambazo zitafanyika kila baada ya miaka miwili(2) katika Mkutano Mkuu wa Kikundi wa mwaka. Kama ifuatavyo:-

*7.1 Mwenyekiti na Makamu Mwenyeki wa kikundi.*

(i) Watachaguliwa kwa kura ya siri.

(ii) Kutoka miongoni wa wajumbe wa kikundi yatapendekezwa majina matatu na kupigiwa kura kwa pamoja, ambapo Mwenyekiti na makamu wake watapatikana kutokana na wingi wa kura utakao patikana. Ambapo atakaye pata kura nyingi zaidi ya mwenzake ndiye atakuwa amechaguliwa kama Mwenyekiti wa kikundi na atakayefutia kwa wingi wa kura atakuwa Makamu Mwenyiki.

### *7.2 Katibu wa Kikundi*

(i) Atachaguliwa kwa kura ya siri.

(ii) Kutoka miongoni mwa wajumbe wa kikundi yatapendekezwa majina matatu na kupigiwa kura kwa pamoja. Katibu atapatikana kutokana na wingi wa kura atakazopata, ambapo atakaye pata kura nyingi zaidi ya mwenzake ndiye atakuwa amechaguliwa kama Katibu wa kikundi. Atakayefutia kwa wingi wa kura atakuwa Katibu Msaidizi

### *7.3 Mweka Hazina wa kikundi*

(i) Atachaguliwa kwa kura ya siri.

(ii) Kutoka miongoni mwa wajumbe wa kikundi yatapendekezwa majina matatu na kupigiwa kura kwa pamoja. Mweka hazina atapatikana kutokana na wingi wa kura atakazopata. Atakaye pata kura nyingi zaidi ya wote ndiye atakuwaamechaguliwa mweka hazina wa kikundi.

## SURA YA NANE

### *8.0 KIINGILIO NA ADA*

Kutakuwa na kiingilio na ada mbali mbali ambazo zimeainishwa kwenye katiba ya kikundi . Kiingilio na ada hizo ni kama ifuatavyo:

1. Kiingilio kwa wanachama shilingi ……………….
2. Ada ya kila mwezi kwa kila mwanachama shilingi ………………………
3. Ada nyingine kama itakavyoamuliwa na wanachama kufuatana na katiba ya kikundi.

### *8.1. Faini za kikundi*

1) Kuchelewa kwenye vikao faini shilingi 2,000/=
2) Kutohudhuria kikao bila sababu ya msingi shilingi 5,000/=
3) Faini ya shilingi 5, 0000/= italipwa na mwanachama aliyeshindwa kuwajibika au kutoshiriki kazi za Kikundi.
4) Kuchelewa kwenye kazi za Kikundi bila sababu za msingi faini shilingi 2, 000/=
5) kulipa mkopo ndani ya muda uliopangwa faini itakuwa shilingi 20,000/=
6) Faini ya shilingi 10,000/= itatozwa kwa mwanacha asiyelipa ada ya miezi 2 mfulululizo.

### *8.2. Matumizi ya Faini*

a) Kuendesha vikao vya kikundi na kufanya uwekezaji.
b) Gharama za uendeshaji wa kikundi kama zitakavyowasilishwa na uongozi na kuidhinishwa na mkutano wa wanachama.
c) Shilingi 2,000/= kwa mwezi zitalipwa kwa viongozi watendaji ambao ni Mwenyekiti, katibu na mtunza hazina ili kurahisisha uratibishaji wa shughuri za vikao kama vile utoaji wa taarifa. Gharama hizi zaweza kuamriwa vinginevyo kwenye vikao vya wanachama.

### *8.3. Mgao wa Mapato*

1) Ada ya mwanachama iliyolipwa toka ajiunge. Fao hili litamlenga mwanachama atakayejitoa au kutolewa.
2) Faida au hasara itokanayo na uwekezaji. Gawio litakuwa theluthi 2/3 ya faida yote na theluthi 1/3 itabidi kuwa sehemu ya mtaji wa kikundi
3) Mgao wa faida au hasara utaamuriwa baada ya taarifa ya mapato na matumizi kutolewa na kamati ya kikundi. Kamati itatoa mapendekezo kuwa faida iliyopo inatosha kutoa gawio kwa mwanachama au hasara iliyopatikana inatakiwa ipunguzwe katika mtaji au kuweka kiwango cha pesa kitakachogawiwa kwa kila mwanachama.

4) Mwanachama asiyelipa michango yake mfululizo kwa miezi mitatu atakuwa amekosa haki ya kupata huduma zilizoainishwa kwenye kifungu hiki cha mgao wa mapato

## SURA YA TISA

### *9.0. UTUNZAJI FEDHA BENKI*

Kikundi kitatunza fedha zake kwenye benki itakayopitishwa na Mkutano Mkuu.

Fedha zitatolewa kwenye akaunti kwa mujibu wa taratibu zilizo wekwa kwenye kanuni za fedha za kikundi.

## SURA YA KUMI

### *10.0. UENDESHAJI WA MIRADI YA VIKUNDI*

Kikundi kitaendesha miradi yake kama ifuatavyo:

1. Kikundi kitaendesha mradi wa Pamoja wa Kikundi na mradi wa mtu mmoja
2. Ikitokea kuwa wanakikundi wanahofu juu ya uendeshaji wa mradi wa Pamoja wa kikundi basi wanaruhusiwa kukukopa mkopo wa mmoja mmoja na kila mtu kufanya mradi wake.
3. Ikitokea mwanakikundi ameshindwa kufanya rejesho wanachama waliobaki wanamlipia kwani mikopo hii haina dhamana hivyo kuwepo katika kikundi ndiyo dhamana yenyewe.
4. Kila mwanachama anawajibika kuweka akiba kulingana itakavyoamuliwa na mkutano mkuu wa kikundi ikilinganishwa na faida itakayotokana na mradi wa kikundi ama miradi ya wanakikundi

### 10.1 MKOPO WA KIKUNDI

Kikundi hiki kinategemea Kuomba Mkopo wa Halmashauri 10% na Mikopo ya Taasisi za fedha kama Benki nk.

### 10.2 DHAMANA YA MIKOPO

Wanachama wa Kikundi hiki wanatambua kua Kikundi hiki ni Dhamana kwa MKOPO wowote utakaoombwa na Kikundi.

### 10.3 UREJESHAJI WA MIKOPO

a) Wanachama wanatambua kuwa wana wajibu wa kufanya Marejesho ya Mkopo ulioombwa na Kikundi hiki

b) Wanachama wanatambua kuwa wamebeba dhamana kukamilisha Marejesho wote pale itakapotokea mwanachama mmoja kashindwa kufanya marejesho kwa wakati kwa sababu mbalimbali kama vile AJALI, KIFO, au Kukimbia nje ya Mkoa.

**SURA YA KUMI NA MOJA**

***11.0. UTATUZI WA MIGOGORO***

Ufuatao ni utaratibu wa kikundi kutatua migogoro itakayo jitokeza ndani ya kikundi:

Migogoro yote ya kikundi itatatuliwa na Kamati ya Nidhamu. Kama Mgogoro huo utashindikana kutatuliwa na Kamati ya Nidhamu mgorogoro huu utapelekwa

(i) Afisa maendeleo ya Jamii wa Kata

(ii) Kupelekea mgogoro huo kwa Ofisi inayofanya utambuzi wa vikundi, kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

(iii) Kupeleka mgogoro mahakamani kwa kufuata taratibu za kisheria.

Gharama za utatuzi wa mgogoro au shauri lililofunguliwa zitalipwa na aliyefungua/ waliofungua mgogoro au shauri hilo. Kikundi hakitahusika na gharama zozote za usuluhishi wa mgogoro husika.

(iv) Na endapo mwanachama/ wanachama watakataa kufuata makubaliano ya utatuzi wa shauri, basi watakuwa wamejifukuzisha uwanachama wao wenyewe /mwenyewe/na kupoteza haki zao za msingi.

**SURA YA KUMI NA MBILI**

***12.0 KUBADILI KATIBA.***

Mabadiliko yeyote ya katiba yatafanyika baada ya kupitishwa na mkutano mkuu wa kikundi wa mwaka ambao unafanyika mara moja kwa mwaka. Mabadiliko yatapitishwa kwa kupigiwa kura ya wazi na zaidi ya asilimia 80% ya wanachama wote waliohai. Katiba itakuwa inafanyiwa marekebisho na kupitishwa upya kila baada ya miaka mitatu, au pale ambapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo

**SURA YA KUMI NA TATU**

***13.0. KUVUNJIKA KWA KIKUNDI.***

(i) Kikundi kitakuwa kimevunjika endapo asilimia 90% ya wanachama hai watapiga kura ya ndio ya kuvunja kikundi katika mkutano mkuu wa kikundi.

(ii) Endapo kikundi kitafutwa na Ofisi ya utambuzi wa vikundi.

(iii) Endapo kikundi kitavunjika kila mwanachama atakuwa na haki sawa ya kurudishiwa michango yake kulingana na hali ya fedha itakavyokua. Mali yote iliyopatikana itagawanywa sawa kwa kila mwanachama.

**SURA YA KUMI NA NNE**

***14.0 HITIMISHO:***

Katiba hii imesomwa, kujadiliwa na kupitisha na wanachama wote leo Tarehe…………

**MAJINA YA WANACHAMA WAANZILISHI WA KIKUNDI CHA …………………………**

| Na | JINA | CHEO | NAMBA YA SIMU | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |

**Mwanasheria**

**Jina………..………………………………………..**
**Saini……………………………………………...**